Mzazi au Mlezi Mpendwa,

Ili kuhakikisha kuwa mtoto wako yuko tayari kwa shule, Msimbo wa Afya na Usalama California Kitengo cha 124085, unahitaji kuwa mtoto wako awe na uchunguzi wa kiafya ndani ya siku 90 baada ya kujiunga na gredi ya kwanza. Vipimo vya afya ambavyo vimekamilishwa ndani ya miezi 18 kabla ya mtoto wako kujiunga na gredi ya kwannza pia vinatimiza mahitaji haya. Uchunguzi wa afya unatolewa katika umri mdogo ili kugundua matatizo yoyote yanayoweza kuhitilafiana na kusoma. Utambulisho na matibabu ya mapema ni muhimu kwa sababu tatizo la kiafya ambalo halijagunduliwa linaweza kukwaza maendeleo ya mtoto shuleni.

**Peleka Ripoti ya Uchunguzi wa Afya ya Usajili Shuleni iliyoambatishwa hapa kwa mhudumu wa afya ya mtoto wako, au mhudumu wako wa afya akamilishe fomu ili kuthibitisha kuwa vipimo vilikamilishwa ndani ya miezi 18 baada ya mtoto wako kujiunga na gredi ya kwanza. Iwapo huwezi kumpeleka mtoto wako katika uchunguzi huu unaohitajika, tafadhali onyesha sababu ya hali hii katika Sehemu ya fomu hii ya Kuondolewa kwa Uchunguzi wa Kimatibabu. Fomu zilizokamilishwa lazima zirejeshwe katika shule ya mtoto wako kufikia tarehe 30 Novemba.**

Iwapo unahitaji usaidizi wa kupata mhudumu wa afya ili kukamilisha mahitaji haya, unaweza kuwasiliana na mojawapo ya rasilimali zilizoorodheshwa hapa chini.

Centro Medico El Cajon - (619) 401-0404
133 W Main St, Suite 100, El Cajon, CA 92020
Chase Avenue Family Health Center - (619) 515-2499
1111 W. Chase Ave, El Cajon, CA 92020
La Maestra Community Health Center - (619) 280-4213
165 S. First., El Cajon, CA 92019
Neighborhood Healthcare - (619) 440-2751
855 East Madison Avenue, El Cajon, CA 92020

Sheria inatambua umuhimu wa afya katika kusoma. Uchunguzi wa afya husaidia kuhakikisha kuwa mtoto wako ameanza shule akiwa na afya nzuri na yuko tayari kusoma.

Tafadhali kumbuka, sheria ya California inahitaji shule zidumishe faragha ya taarifa ya afya ya wanafunzi. Utambulisho wa mtoto wako hautahusishwa na ripoti yoyote itakayozalishwa kutokana na mahitaji haya. Iwapo una maswali yoyote kuhusu mahitaji ya Uchunguzi wa Afya wa Usajili Shuleni, tafadhali wasiliana na Ofisi ya Afya katika shule.

Wako mwaminifu,
Jennifer Shultz, MSN, RN, SNSC

Jennifer Shultz (MSN, RN, SNSC) | Mratibu, Huduma za Uuguzi na Afya| shultzj@cajonvalley.net | P:619.588.3297 |F:619.588.3015